





Fana na familia yake wanaishi katika mji wa Debre Birhan nchini Ethiopia. Fana ni mwanafunzi wa darasa la tatu. Ana roho nzuri na mwenye hekima.




Fana anawapenda  
wanyama. Ana paka mmoja,  
kuku wawili, mbuzi na njiwa.  
Anakuwa nao kwa muda  
mrefu akiwalisha na  
kucheza nao.



Siku moja, Fana na wenzake walikuwa wakicheza uwanjani shulenii. Fana aliwaona watoto wakiwarushia njiwa mawe.

Alijiuliza, "Mbona wanawaumiza njiwa?"



Aliacha kucheza akakimbia  
kuelekea mahali watoto  
wale walikokuwa.

Mwanzoni, wenzake  
hawakuelewa kilichokuwa  
kitendeka. Walimfuata.  
Fana aliwakemea wale  
watoto, "Acheni kurusha  
mawe."



Wale watoto watukutu walitoroka.

Fana aliwashika njiwa waliojeruhiwa. Aliona majeraha kwenye mbawa zao. Aliamua kuwapeleka nyumbani kuwalinda.



Fana aliwalisha njiwa. Jioni aliisimulia familia yake alichokiona na kufanya siku ile na jinsi alivyowaokoa njiwa.



Asubuhi, Fana na wazazi wake welienda katika kliniki kupata dawa za kuwaponya njiwa.

Baada ya siku chache, njiwa walipona majeraha yao. Fana alifurahi sana.



Kila mara, Fana aliwaambia  
marafiki zake,  
“Ninawapenda wanyama.  
Wanyama wana manufaa  
kwetu na ni marafiki zetu.  
Lazima tuwalinde na  
kuwahifadhi.”